



MTIHANI

Kundi la kwanza la wakaguzi walioidhinishwa wa ulaghai wakamilisha kozi ya KASNEB

UK 3



MADINI

Kenya kuanzisha kiwanda kikubwa zaidi cha usindikaji wa granite katika Emuhaya, Vihiga

UK 8

KILIMO

Wataalam wapigia debe matumizi ya viua magugu kwa mavuno mengi na udhibiti rahisi wa magugu



UK 14

Julai 30, 2024

MyGov. TATHMINI YAKO YA WIKI

www.mygov.go.ke

TOLEO No. 5/2024-2025

Akiba ya nafaka Kenya kuzidi mahitaji kufuatia mavuno bora



Paul Rono

Ziada hii inahusu hifadhi ya magunia milioni 36.6 na makadirio ya magunia milioni 1.08 ya kilo 50 yalivyotabiriwa kuagizwa kutoka nje katika kipindi cha miezi mitatu ijayo, kulingana na ripoti ya Salio ya Hifadhi ya Chakula Kitaifa

NA WANGARI NDIRANGU(KNA)

Kutakuwa na ziada ya mahindi ya takriban magunia milioni 31.07 ya kilo 50 kufikia mwisho wa Agosti 2024, kulingana na Ripoti ya Idara ya Kilimo, Chakula na Lishe ya Serikali.

Ziada hii ni kutokana na hifadhi ya magunia milioni 36.6 na makadirio ya magunia milioni 1.08 ya kilo 50 yaliyokadiriwa kuagizwa kutoka nje katika kipindi cha miezi mitatu ijayo,

kulingana na ripoti ya ya Hali ya Salio ya Hifadhi ya Chakula Kitaifa.

Katibu wa Kilimo Paul Rono anasema kuwa hali ya hifadhi ya taifa na makadirio ya matumizi yanaonyesha kuwa takriban magunia milioni 24.5 ya mahindi yatafunwa kutoka kwa mazao ya mvua ndefu katika kaunti za nyanda za chini, zenye joto zaidi, zikiwemo

ENDELEA UK 2



32 M	Sh2.5b	25,000	Sh66-milioni	300	1,500	
Takwimu za Wiki	Mahindi ya ziada yanayotarajiwa (mifuko ya kilogramu 50) ifikapo mwisho wa Agosti 2024	Gharama ya kiwanda cha kuchakata granite huko Emuhaya katika Kaunti ya Vihiga	Idadi ya miti wafanyakazi wa Wizara ya Afya wanalenga kupanda Pokot Magharibi	Gharama ya kituo cha afya cha kisasa cha Hemingways kitajengwa Maasai Mara.	Walemavu Manderu waliopokea vifaa vya uhamaji kutoka kwa kaunti	Vijana walio katika mazingira magumu ambao wamefunzwa Kaunti ya Tharaka Nithi



Katibu wa Uchukuzi Mohamed Daghar (Aliyekaa) alipopokea na kukagua makochi 20 mapya ya Huduma kwa Abiria ya Madaraka Express katika Bandari ya Mombasa.

Shirika la Reli la Kenya lazindua makochi 20 mpya za kisasa ya Madaraka Express

NA SADIK HASSAN (KNA)

Shirika la Reli la Kenya limeagiza makochi 20 mapya ya kisasa ya abiria ili kuimarisha Huduma za Abiria katika Madaraka Express kati ya jiji la pwani la Mombasa na Nairobi.

Takwimu za Shirika la Reli la Kenya zinaonyesha kuwa abiria milioni 12 wamesafirishwa tangu kuanzishwa kwa huduma ya treni ya abiria ya Madaraka Express mnamo 2017.

Makochi hayo mapya 20 ya kuhudumia abiria yaliyoinduliwa na Katibu wa Uchukuzi, Mohamed Daghar, yanajumuisha makochi kumi ya daraja la kwanza yaliyoboreshwa, makochi manne ya

daraja la juu, gari moja la kulia chakula na makochi manne ya daraja la kwanza yenye lengo la kuboresha huduma na kukidhi matarajio ya wateja.

Ili kuboresha zaidi uzoefu wa wateja, katibu Daghar alibainisha kuwa mipango inaendelea ya kuweka Wi-Fi kwenye treni na kuboresha mifumo ya ukataji tiketi.

Makochi manne ya daraja la

12 milioni

Abiria waliosafirishwa tangu kuanzishwa kwa huduma ya treni ya abiria ya Madaraka Express mnamo 2017.

kwanza yameundwa ili kuhakikisha faraja na urahisi kwa abiria. Yana mpangilio bora wa kuketi, na kila kochi lina idadi ya abiria 28, inahakikisha nafasi ya kutosha ya miguu na nafasi ya kibinafsi.

Yameboresha ubebaji wa mizigo kwa abiria walio na mizigo ya ziada, viti vinavyoweza kubadilishwa ambavyo vinaweza kugegemea kikamilifu, kutoa utulivu na faragha, na vipengele vya ubunifu kama vile vibao vya dirisha za otomatiki na viti vinavyozunguka.

"Hii ni ya kwanza ya aina yake nchini Kenya na pengine katika ukanda huu. Haya ni makochi ya

ENDELEA UK 2

Akiba ya nafaka Kenya kuzidi mahitaji kufuatia mavuno bora

ENDELEA KUTOKA UK 1

Bomet, sehemu za Narok, Nyamira na sehemu za Migori, ambapo upanzi wa mazao ulianza mapema Januari.

“Hifadhi iliyopo inatosha kwa nchi hadi mavuno yajayo ya mvua ndefu kuanzia Agosti 2024 katika kaunti nyingi,” alisema.

Katibu alibainisha kuwa ripoti ya hali ya ngano iliyotarajiwa kufikia mwisho wa Agosti 2024 inaonyesha ziada ya magunia milioni 10.2 ya kilo 50, ikichukuliwa kuwa sekta ya kibinafsi iliagiza magunia milioni 8.7 ya kilo 50 katika miezi mitatu ijayo.

Ripoti ya Mchele inayotarajiwa kufikia mwisho wa Agosti 2024 inaonyesha ziada ya mifuko milioni 4.1 ya kilo 50 kulingana na akiba ya magunia milioni 3.3 ya kilo 50.

Ripoti ya hali ya maharagwe inayotarajiwa kufikia mwisho wa Julai 2024 inaonyesha ziada ya magunia milioni 10.3 ya kilo 50 kulingana na akiba ya magunia milioni 3.4, takriban magunia

270,000 ya makadirio ya uagizaji bidhaa kutoka kwa sekta binafsi katika kipindi cha miezi mitatu ijayo, na takriban magunia milioni tisa ya kuvunwa mapema Juni na Julai. Katibu alibainisha kuwa uagizaji wa mahindi mwezi Mei ulipungua kutoka 523,771 (magunia ya kilo 50) mwezi Aprili hadi 516,151 (magunia ya kilo 50) na ikilinganishwa na 633,555 (magunia ya kilo 50) yaliyoagizwa kutoka nje mwezi Machi.

“Mengi ya mahindi yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi yalitoka Tanzania, na kiasi kikubwa kilitoka Uganda,” Dkt Rono alisema.

Aliongeza kuwa kiasi cha maharagwe yaliyoingizwa nchini mwezi Mei kiliongezeka mara dufu kutoka magunia 5,153 (kilo 50) hadi magunia 11,931 (kilo 50) yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi mwezi Aprili. Lakini bado, jumla ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje ni mdogo sana ikilinganishwa na miaka iliyopita, alisema.

Aidha, kiasi cha mchele ulioagizwa ku-

toka nje mwezi Mei kilipungua zaidi hadi 352,300 (magunia ya kilo 50) ikilinganishwa na 610,020 (magunia ya kilo 50) yaliyoagizwa mwezi Aprili ikilinganishwa na milioni 1.185 (magunia ya kilo 50) yaliyoagizwa mwezi Machi. Kulingana na katibu, Ripoti ya hivi karibuni Utoshelevu wa Chakula na Lishe umeimarika kuanzia Mei. Alisema vyakula vikuu vingi vinapatikana katika familia na sokoni.

“Bei za mazao ya msingi, hasa nafaka na kunde, ziliendelea kushuka mwezi Mei kwani baadhi ya wakulima ambao walikuwa waki-hifadhi zao waliamua kupeleka sokoni,” Dkt Rono alisema.

“Kupungua taratibu kwa bei ya chakula muhimu kunaendelea kuborisha upatikanaji wa chakula kwa familia, huku uagizaji kutoka nje ya mipaka ya matoraji ya mavuno kutoka msimu wa sasa zikiwa na uwezekano wa kudemisha kushuka kwa bei katika miezi ijayo,” katibu Rono alieleza.

Shirika la Reli lazindua makochi 20 mpya ya Madaraka Express

ENDELEA KUTOKA UK 1

kustarehesha ambayo yana vipengele tofauti vya usaidizi ambavyo vinasaidia aina tofauti xa wateja wakisafiri,” alisema katibu Dagar katika uwanja wa Port Reitz Freight Yard mjini Mombasa. “Viti vimegemea kikamilifu kwenye kitanda cha gorofa, na kuna sehemu za kuchaji vifaa vyako vya rununu,” akaongeza.

Katika Daraja la Kawaida, abiria hawataketi tena wakitazamana. Badala yake, mpan-gilio wa viti watatu kwa-wawili katika upana wa kochi utakuwa na abiria wanaotazama hima kituo cha kuondoka au wanakoeleka.

“Kilichoongoza kutoka kwa maoni tuliyoapokea ilikuwa kutoweza kuchaji simu. Sasa tuna furaha kutangaza kwamba tuna vituo vinne vya kuchaji katika kila mpangilio wa viti. Tunahakikishia sasa kwamba unaweza kuchaji simu zako,” alifanua katibu Dagar.

Makochi pia sasa yana eneo la kubadilisha wa-



Katibu wa Uchukuzi Mohamed Dagar alipoindua makochi 20 mpya ya Huduma ya Abiria wa Madaraka Express katika Bandari ya Mombasa.

toto kwa wakati wa safari na meza zinazokunjwa na mifuko vitini kuweka vitu vidogo.

“Pia tunapokea gari lenye nguvu zaidi. Tuli-kuwa tunabeba makochi 13 kwa gari moja, kwa gari jipya ambalo tumepokea tunaweza kubeba makochi 20,” alisema katibu. Katibu pia alisisitiza dhamira ya serikali ya kuimarisha reli ya zamani (MGR) ili kuinganisha na kuimarisha uchukuzi.

Mipango iko katika hatua ya juu ya kurekebisha reli ya Ruiru mo-

jawapo ya njia za reli za abiria zenye shughuli nyingi zaidi kupitia usaidizi wa Benki ya Dunia chini ya Mradi wa Uboreshaji wa Uhamaji Mijini wa Kenya.

KRC kufikia sasa imejenga vituo 20 na vitano vya usafiri jijini Nairobi na Mombasa mtawalia ambavyo vinaunganishwa na vituo vya SGR katika miji hiyo miwili. “Tumedhamiria kuhakikisha kuwa wateja wetu wanaendelea kuzunguka Kenya bila mshono.



NOTISI YA TENDA

Kenya National High Authority (KeNHA) ni Shirika la Serikali lililoanzishwa chini ya Sheria ya Barabara za Kenya, 2007, likiwa na jukumu la Usimamizi, Ukarabati wa Uendelezaji na Utunzaji wa Barabara za Kitaifa.

KeNHA inakaribisha zabuni zilifungwa kutoka kwa Watoa Huduma wanaostahiki kwa zabuni ifuatayo.

S/No.	Nambari ya Tenda	Maelezo ya Tenda	Kufunga/Kufungua/Saa/Eneo
1.	KeNHA/2787/2024	Utoaji wa Huduma za Kibinafsi za Usalama kwa Ofisi Kumi za Kanda za KeNHA (Nambari 10) na Ofisi za Ukanda	Agosti 16, 2024 at 11.00am. Makao Makuu ya KeNHA, Barabara Plaza, Jomo Kenyatta International Airport (JKIA) Nairobi, Off Mazao Road, Block C - 2 nd Floor Board Room.

Seti kamili ya hati ya zabuni inaweza kupatikana na Wazabuni wanaovutiwa bila malipo kwa kupakua kutoka tovuti ya KeNHA: www.kenha.co.ke au Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP): www.tenders.go.ke au kutoka Ofisi ya KeNHA JKIA Barabara Plaza Block C, Ghorofa ya Pili ya Ofisi ya Usimamizi wa Ugavi wakati wa saa za kawaida za kazi baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa ya Kshs, 1,000.00 (shilingi elfu moja pekee) kama hundi ya benki inayolipwa kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara Kuu ya Kenya.

Kutakuwa na ziara ya lazima ya tovuti kabla ya zabuni kama ilivyobainishwa katika hati ya zabuni iliyopakwa kwenye tovuti ya KeNHA na PPIP.

Wazabuni wanahimizwa kupakua hati ya Zabuni kutoka kwa tovuti zilizo hapo juu ili kupunguza mson-gamano katika Ofisi za KeNHA.

Wazabuni wote wanaovutiwa wanatakiwa kuangalia mara kwa mara tovuti ya Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara za Kenya: www.kenha.co.ke na Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP) kwa nyongeza yoyote ya zabuni au ufafanuzi ambao unaweza kutokea kabla ya tarehe ya kuwasilisha.

Naibu Mkurugenzi (Idara ya Ugavi)
Kwa Niaba ya: MKURUGENZI MKUU

For all your enquiries email us on: complaints@kenha.co.ke Toll Free Line: 0800-211-244 Customer Care: 0700 423 606 #RoadSafetyStartsWithYou

@KeNHAKenya

Website: www.kenha.co.ke

Kenya National Highways Authority

ISO 9001:2015 Certified



FINANCIAL YEAR 2024-2025 APPLICATIONS FOR POSTGRADUATE SCHOLARSHIPS

The Higher Education Loans Board invites applications for the 2024-2025 Postgraduate partial scholarships from Kenyan students enrolled for Masters and PhD programs in local Public or Private Universities recognized by the Commission for University Education [CUE].

The value of the scholarship award is **Kshs.200,000** and **Kshs.450,000** for Masters and PhD programs respectively, tenable for 2 years in respect of the Masters Program and 3 years for the PhD.

ELIGIBILITY CRITERIA:

- Letter of Admission into a full or part time program in a local public or private university recognized by the Commission for University Education [CUE].
- Minimum of **Second-Class Upper Division**.
- Preference will be given to applicants undertaking Science, Technology, Engineering, Agriculture and Mathematics (**STEAM**) courses.
- If HELB loan beneficiary, the applicant **MUST** be repaying his/her loan or has cleared the same.

HOW TO APPLY:

- Applicants should register, access, and duly complete the 2024/2025 Postgraduate Scholarship Application. The form can be accessed via www.helb.co.ke.
- Submit online the duly completed form.

NOTE

- The applicant shall be Prompted to pay **A non-refundable** application fee of KShs.3,000 via E-CITIZEN once they click on the payment tab on the portal.
- Do not pay any individual to process your HELB Postgraduate Scholarship Application.
- Persons with Special needs and from Marginalized counties are encouraged to apply
- The Application Closes on **31st August 2024**

EMPOWERING DREAMS

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way USSD *642#
+254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE

Athletics Kenya yafungua afisi ya kwanza kabisa mjini Eldoret

NA EKUAM SILVESTER NA JUDY TOO(KNA)

Chama cha Riadha Kenya (AK) kimezindua afisi yake ya kwanza kabisa mjini Eldoret, Kaunti ya Uasin Gishu, ili kuhakikisha wanariadha wanaweza kupata huduma kwa urahisi na kwa gharama nafuu wanapokuwa wakifanya mazoezi kwenye kambi zao.

Hapo awali, wanariadha walilazimika kuingia gharama za usafiri kwani walilazimika kusafiri hadi Nairobi kupata huduma, zikiwemo usajili, miongoni mwa zingine.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa afisi hiyo mpya mjini Eldoret, Rais wa AK Jackson Tuwei alidokeza kuwa afisi hiyo, iliyoanzishwa kupitia juhudi za Kamati ya Kupambana na Matumizi ya Dawa za Kulevya, ilikuwa na manufaa kwa wanariadha hao.

Alitangaza kuwa usajili utaanza mara moja, kuanzia Julai 24, 2024, na kuwahimiza wanamichezo kutoka eneo zima kutembelea ofisi hiyo ili kupata

huduma zote.

“Kwa nini tuwe afisi hii ya Eldoret kwa Riadha Kenya? Kwanza, hiki ndicho kitovu cha riadha. Tunataka wanariadha wetu wapate uangalizi wa karibu katika masuala ya huduma zetu, kama vile stakabadihi, usajili na mapendekezo, huku wakizingatia mafunzo,” A alieleza Rais huyo wa AK..

“Tuliona ni muhimu kwetu kufungua ofisi hii hapa ili kuwasaidia wanariadha, wafanyakazi wa usaidizi wa wanariadha na watu wengine ambao wanaweza kuhitaji habari kuhusu mahitaji ya huduma za AK.

Tunataka kuwarahisishia wanariadha kupata hati hizi kwa njia inayoweza kudhibitiwa zaidi,” Tuwei alieleza.

Huku akibainisha kuwa Kenya ni miongoni mwa nchi safi zaidi duniani katika masuala ya utumiaji dawa za kususimua misuli, Tuwei alizidi kuwataka wananchi wasisahau kutambua juhudi za magwiji waliochangia maendeleo ya riadha humu nchini.

Hemingways Collection na Maa Trust wazindua kituo cha afya cha kisasa

NA BERNADETTE KHADULI(KNA)

Kampuni ya Hoteli za Hemingways Collection imeshirikiana na Maa Trust kujenga kituo cha afya cha kisasa cha Sh66-milioni katika Maasai Mara Kaunti ya Narok.

Kituo hicho kitajumuisha chumba cha upasuaji, kitengo cha watoto wachanga wanaohitaji uangalizi maalum, uzazi ili kutoa mazingira salama kwa mama wawawazito na walio katika hatari kubwa baada ya kujifungua, akina mama wachanga na vijana.

Mnamo 2023, Maa Trust ilitatibu uchangishaji wa fedha za ujenzi, vifaa, na uendeshaji wa kituo cha Afya ya Mama na Watoto (MNCH) katika Kituo cha Afya cha CHP Talek.

Ujenzi wa kituo hicho ulikamilika, na kilianza kufanya kazi mwaka huu kupitia ushirikiano kati ya vikundi mbalimbali vya washirika, ikiwa ni pamoja na Hemingways Collection, M-Pesa Foundation, Gertrude's



Hospital Foundation, John na Jennifer Guistina Family Fund, na Serikali ya Kaunti ya Narok miongoni mwa wengine.

Katika taarifa iliyoitumwa kwa vyombo vya habari, Afisa Mkuu Mtendaji wa Hemingways Collection Bw Ross Evans alitangaza kwamba Hemingways ilijitolea kutoa mchango wa Sh260 kwa kila kitanda kimoja usiku katika Hemingways Nairobi na Sh650 kwa Hemingways Ol Seki kwa kila kitanda usiku ili kufa-

dhili shughuli zinazoendelea za MNCH.

“Kufikia sasa tumechangisha Sh1.9 milioni (dola 14,500) kwa kituo hiki na tunawahimiza wageni wetu walio Hemingways Ol Seki kutembelea Makao Makuu ya Maa Trust ili kujifunza zaidi kuhusu shirika na athari kubwa kwa jamii na uhifadhi katika mfumo wa ikolojia wa Mara,” Evans alisema.


Aliongeza kuwa ufaadhili huo pia utasaidia mishahara ya madaktari

na wauguzi ili kuhakikisha kuwa kina mama na watoto wachanga wanapata huduma bora za matibabu.


Kituo hicho kimeundwa kuhudumia wawawazito walio katika hatari kubwa ikiwa ni pamoja na kina mama vijana. Maa Trust inatarajia kuwa itachukua miaka miwili ili kufikia uendelevu wa kifedha.

Katika hotuba yake, Afisa Mkuu Mtendaji wa Maa Trust Dkt Crystal Mogensen alisema kituo cha Afya ya Mama na Watoto (MNCH) ni mradi wake binafsi unaotokana na matatizo aliyoyapata alipokuwa akijifungua Maasai Mara.

“Mnamo 2021, niliingia katika leba wiki 10 kabla ya wakati wake hapa Maasai Mara. Ilikuwa tu kwa sababu ya kuhamishwa kwa helikopta hadi Nairobi ambapo mwanangu alinusurika. Pia nimepitia ujauzito mwingine ulio hatarini zaidi na binti yangu ambaye alizaliwa salama, wiki nne tu kabla ya wakati,” Dkt Mogensen alikumbuka.



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL



KNEC is ISO 9001:2015 Certified

NOTISI YA TENDA

Baraza la Kitaifa la Mitihani la Kenya (KNEC) ni Shirika la Serikali lililoanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Kitaifa la Mitihani la Kenya Nambari 29 ya 2012. Baraza hilo lina mamlaka ya kufanya tathmini na mitihani ya kitaifa katika viwango vya msingi na vya elimu ya juu na kuwaidhinisha wanafunzi.


1.0 KNEC inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa Wazabuni wanaostahiki kwa Zabuni zilizo hapa chini:

S/No.	NAMBARI YA TENDA	MAELEZO YA TENDA	KUNDI
1.1	KNEC/RFP/2024-2025/01	Utoaji wa Ushauri wa Vyombo vya Habari na Huduma za Usaidizi	Wazi
1.2	KNEC/ONT/2024-2025/11	Utoaji wa Mafuta, Mafuta, Vilainishi na Bidhaa Zinazohusiana kwa Magari ya KNEC yanayotumia Kadi za Kielektroniki za Mafuta kwenye Mkataba wa Mfumo wa miaka miwili.	Wazi
1.3	KNEC/ONT/2024-2025/12	Utoaji wa Msaada wa Mfumo wa SAGE AccPac na Huduma ya Matengenezo	Wazi
1.4	KNEC/ONT/2024-2025/13	Utoaji wa Huduma za Kinga ya Matengenezo na Urekebishaji kwa Mfumo wa Kiyoyozu wa 60,000 wa BTU.	Wazi
1.5	KNEC/ONT/2024-2025/14	Kuhudumia, Ukarabati na Utunzaji wa Vifaa vya Ugavi wa Umeme usioingiliwa (UPS) kwa mkataba wa miaka miwili.	Vijana
1.6	KNEC/ONT/2024-2025/15	Matengenezo na Urekebishaji wa Mifumo ya Mabomba kwa mkataba wa miaka miwili	Vijana
1.7	KNEC/ONT/2024-2025/16	Utoaji wa Huduma za Ukusanyaji takataka chini ya mkataba wa miaka miwili	Kina mama
1.8	KNEC/ONT/2024-2025/17	Utoaji wa Huduma za Ukusanyaji wa Mapipa ya Usafi mkataba wa miaka miwili	Kina mama

2.0 Wazabuni wanaostahiki wanaweza kupata hati za zabuni kutoka kwa tovuti zifuatazo: www.knec.ac.ke au www.supplier.treasury.go.ke au www.tender.go.ke

3.0 Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha itakuwa kulingana na tarehe zilizotolewa katika hati za zabuni husika.

AFISA MKUU MTENDAJI








TANGAZO LA ZABUNI

Baraza la Wakimbizi la Denmark (DRC) linatekeleza mradi wa Mfuko wa Udhambi wa Sekta ya Maji (WaterFund) katika Kaunti Ndogo za Fafi na Dadaab, Kaunti ya Garissa uliopewa jina la “Usimamizi Endelevu na Upatikanaji wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Mpango wa ASALS (SWASAP)” unaongwa mkono na Ubalozzi wa Kifalme. ya Denmark kupitia DANIDA. Mpango huu unalenga kuongeza ustahimilivu wa jamii na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa kupitia matumizi endelevu, ya amani ya maliasili ikijumuisha uboreshaji wa upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika Kaunti zinazolengwa za ASAL. DRC inawaalika wakandarasi wanaovutiwa, wenye uzoefu, wanaotambulika na wenye leseni kuwasilisha ofa (zabuni) zilizofungwa kwa zabuni ifuatayo na tarehe za mwisho za **tarehe 9 Agosti 2024 saa 11 asubuhi**. Mawasilisho yaliyochelewa hayatazingatiwa.

NAMBARI YA TENDA	MAELEZO YA TENDA	WASTAHIKI
DRC/SWASAP/00300763 /23/24	Vifaa vya Kisima, Ufungaji wa Sola, utengenezaji na uwekaji wa Tangi ya Chuma ya Juu ya 100m3, Upanuzi wa Bomba na ua katika Kambi ya Wakimbizi ya Ifo, Kaunti Ndogo ya Dadaab, Kaunti ya Garissa.	Wazi kwa wazabuni wote waliohitimu na wanaovutiwa.

Nyaraka za Zabuni zinapatikana Bila Malipo kwa wazabuni wote waliohitimu na zinaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti ya Baraza la Wakimbizi la Denmark www.drc.ngo. Wazabuni wanaopenda kupata maelezo zaidi au kutafuta ufafanuzi wanaweza kufanya hivyo kwa kutuma barua pepe kwa procurement.ken@drc.ngo

Nyaraka za Zabuni zilizokamilishwa katika bahasha zilizofungwa wazi ziwasilishwe katika nakala mbili- Halisi na nakala zikiwa na alama wazi **“USIFUNGE KABLA” Tarehe 9 Agosti 2024 saa 11 asubuhi** zikionyesha Nambari ya Zabuni na kuwasilishwa kwenye Sanduku la Zabuni la DRC katika Ofisi Kuu ya DRC katika Lower Kabete Road (Makutano ya Barabara ya Ngecha) na kuelekezwa kwa;

Ofisi ya Ununuzi
DRC Afrika Mashariki na Ukanda wa Maziwa Makuu
Barabara ya Kabete ya Chini (Makutano ya barabara ya Ngecha)
S.L.P 14762-00800 Westlands
Nairobi, Kenya

Wazabuni pia watahitajika kusajili maelezo yao wanapoacha zabuni zao. Zabuni zitafunguliwa mbele ya wazabuni au wawakilishi wanaotaka kushuhudia mchakato wa ufunguzi.



Katibu ahimiza Wakenya wanaotafuta kazi ng'ambo kujifua lugha za kigeni

NA CATHERINE KAMAU (PCO)

Katibu wa Leba na Ukuzaji wa Ujuzi, Bw Shadrack Mwadime, amewataka Wakenya wanaotaka kupata nafasi za kazi nje ya nchi kujifunza lugha za kigeni ili kujiandaa kwa kazi ambazo serikali inawatafuta.

Akiwa hutu bina wanafunzi wa matibabu na uuguzi katika chuo kikuu cha Kenya Methodist (KeMU) mjini Meru, Mwadime aliwahakikishia Wakenya kwamba nafasi za kazi zinapatikana nje ya nchi kutokana na makubaliano ya kazi ya nchi mbili yaliyotiwa saina kati ya Kenya na mataifa mengine.

Kwa hivyo, Mwadime alihimiza usimamizi wa KeMU kuanzisha mafunzo ya lugha ya Kijerumani ili kuwawezesha wanafunzi wanaopenda kufanya kazi nchini Ujerumani, kwa kuwa ni sharti katika makubaliano ya kazi ya nchi mbili kati ya Kenya na Ujerumani.

Katibu alisisitiza haja



Katibu Shadrack Mwadime, Naibu Chansela wa chuo kikuu cha KeMU Prof J John Kobia (kulia) akijibu maswali kutoka kwa wanafunzi

ya kazi za miezi sita ya kufundisha lugha ya Kijerumani, hasa kwa wale walio katika sekta ya matibabu, kwani kuingiliana moja kwa moja na wateja na kujua lugha yao ni muhimu.

Mwadime alikiri kuwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Ujuzi imekuwa ikitafuta fursa kwa vijana kwa dhati na kuomba radhi kwa mawasiliano duni kuhusu mipango ambayo imekuwa ikifanyika na inayoendelea kufanywa lakini haijawasilishwa ipasavyo kwa umma.

"Tumefanya na tunaeendelea kufanya mengi kuhakikisha mnapata ajira hapa Kenya

na nje ya nchi, lakini nakubaliana na Rais William Ruto kwamba taarifa hizo hazifiki mashinani inavyotakiwa, na mimi binafsi naomba radhi kwa hilo," Mwadime alisema.

Alitoa mfano wa makubaliano ya kazi kati ya nchi mbili yaliyokamilika na Ujerumani kwa madaktari na wauguzi kufanya kazi nchini humo ambayo yatakamiliwa Septemba mwaka huu.

"Wakati wa mazungumzo, Serikali ya Ujerumani ilitaja upungufu wa wafanyikazi wasiopungua laki mbili na hamsini elfu katika sekta zote zinazohitaji ujuzi

wa matibabu ni kubwa zaidi," katibu alisema.

Akiwa hutu bina wanafunzi hao, Kaimu Katibu wa Uhamiaji wa Kazi Bw Joel Mwanzia ambaye alikuwa ameambatana na Katibu na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kitaifa la Ajira Bi Edith Okoki aliwahakikishia Wakenya kuwa vikwazo na mchakato wa muda mrefu wa kupata kibali cha kufanya kazi nje ya nchi kwa waombaji kitatuliwa.

"Idara ya Uhamiaji wa Leba iliundwa mwaka mmoja uliopita ili kurahisisha uhamiaji wa wafanyikazi katika mashirika, taasisi za umma na za kibinafsi," Bw Mwanzia aliongeza.

Akijibu wanafunzi kuhusu ni kwa nini Wakenya wanakufa katika nchi za Ghuba, jambo ambalo lilitia wasiwasi mkubwa, Bi Edith Okoki aliwashauri Wakenya kuingia katika tovuti ya Shirika la Kitaifa la Uajiri na kutumia tu mashirika ya kibinafsi ya kuajiri yaliyoorodheshwa na shirika hilo.

Mombasa yashirikiana na ILO kupiga vita janga la ajira ya watoto

NA CHARI SUCHE(KNA)

Serikali ya Kaunti ya Mombasa imeeleza kujitolea kwake kushughulikia masuala muhimu yanayosababisha tishio la ajira kwa watoto katika kaunti hiyo kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo na washikaduu wengine.

Kwa kufanya hivyo, Idara ya Utawala wa Umma katika Kaunti itatekeleza vipengele vyote katika Wito wa Kuchukua Hatua wa Mombasa dhidi ya Ajira ya Watoto.

Hii ni pamoja na kuunda sheria na sera wezeshi na vile vile kusaidia mipango ya utekelezaji ili kujenga uwezo wa serikali ya kaunti na washikaduu kushughulikia uajiri wa watoto, uajiri wa kulazimishwa na ulanguzi wa watu.

Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duni-ani (ILO) Coffi Agossou alisema Wito wa Mombasa wa Hatua 2024 ni dhamira kuu ya kushughulikia masuala muhimu zaidi katika ajira ya watoto katika kaunti.

Mpango huu unagusia miongoni mwa mengine, maeneo yote ya kipaumbele chini ya Wito wa Durban wa Kuchukua Hatua 2022, ambao ni mwongozo wa kimataifa wa kushughulikia ajira ya watoto.

Sera ya Mombasa ya kuangamiza Ajira ya Watoto, ambayo kwa sasa inaundwa, huenda ikawa chombo muhimu katika kusaidia uundaji wa miundo na mipango muhimu ya kushughulikia ipasavyo ajira ya watoto nchini.

Agossou alisema ILO, kupitia mradi wa CAPSA, itaendelea kutoa usaidizi wa kiufundi na kifedha kwa Serikali ya Kaunti ya Mombasa ili kuandaa Sera ya Kaunti ya Mombasa kuhusu kuangamizwa ajira ya watoto.

Alisema mradi huo utakuwa ni sera ya kwanza nchini katika ngazi ya kaunti kuhusu ajira ya watoto, na kuingeza kuwa shirika hilo pia litatoa usaidizi kwa kaunti kuanzisha kamati ndogo ya uajiri wa watoto, ambayo itasimamiwa na Kamati ya Ushauri wa watoto ya Kaunti.



FINANCIAL YEAR 2024-2025

UNDERGRADUATE STUDENTS' FIRST TIME SCHOLARSHIP, LOANS & BURSARY APPLICATIONS UNDER THE OLD AND NEW FUNDING MODELS

Higher Education Loans Board in conjunction with Universities Fund invites applications for the First Time 2024-2025 Financial Year Undergraduate Student Scholarship and Loan from Kenyan students placed in public universities by the Kenya Universities and Colleges Central Placement Service [KUCCPS]. Kenyan Students placed or in self-sponsored programmes in Public and Private Universities in Kenya and the East African Community that are recognized by the Commission for University Education [CUE] also qualify to apply for HELB Loan only.

Eligible students for Old Funding Model: Undergraduate Students applying for scholarship and loan for the First-Time and who sat for their KCSE before the year 2022.

Eligible students for The New Funding

Model: Newly placed Undergraduate Students applying for scholarship and loan for the First-Time and who sat for their KCSE in 2022 or 2023 only.

HOW TO APPLY:

1. Visit www.helb.co.ke to access the application portal to register, create and activate account (applicants are advised to use their personal mobile number registered under their name and National Identification Number).
2. Log in, go to apply for Loan/Scholarship or both, click and select the **2024-2025 Undergraduate First Time Scholarship and Loan Application Form**. (you can only apply for both loan and scholarship if you sat for your KCSE in 2022 or 2023 and newly placed by KUCCPS)
3. Read and appraise yourself online on Financial Literacy and appreciate the purpose of Higher Education Financing.

4. Access and fill the Scholarship and Loan application form.
5. Upon successful application and submission of the Scholarship and Loan application online, **YOU ARE NOT** required to print and submit any physical application to us. **(This is a paperless application process)**
6. You will be enabled to track the processing status of your application on the application portal.
7. For any assistance/support, kindly Contact HELB through contactcentre@helb.co.ke

Please ensure that you read, understand, and follow the instructions provided at the beginning of the online Scholarship and loan application process including reading and undertaking the HEF Financial Literacy Programme.

#KaaChonjo, HELB does not charge any fee to access the loan application. Report any form of extortion to authorities.

The closing date for the applications is **31st December 2024**.

EMPOWERING DREAMS

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way USSD *642#
+254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE



FINANCIAL YEAR 2024-2025

UNDERGRADUATE CONTINUING STUDENTS' SUBSEQUENT SCHOLARSHIP & LOAN APPLICATIONS UNDER THE OLD AND NEW FUNDING MODELS

The Higher Education Loans Board in conjunction with Universities Fund invites applications for the **2024-2025 Financial Year Second and Subsequent Undergraduate Scholarship and Loans**, from Kenyan continuing students placed by the Kenya Universities & Colleges Central Placement Service [KUCCPS] and those in Self-sponsored Programs in Public & Private Universities in Kenya and the East African Community that are recognized by the Commission for University Education [CUE].

Eligible students: Undergraduate Continuing Students applying for the **second and subsequent student scholarship and loan**.

How to Apply:

1. Download the **HELB App** from **Google Play Store** or use **USSD Code** by dialing ***642#**
2. Register using your phone number to generate a PIN which you will use to log in.
3. Read, understand, and click to accept the **terms and conditions**.
4. Enter your (first name) as it appears on your national ID card, the ID number and valid email address to complete registration.
5. Click on the **scholarship or loans or loans & scholarship** tab and choose degree. Then click **"apply"** on the Undergraduate second and subsequent scholarship and loan.
6. Read and understand the process tutorial and proceed to read the financial literacy guide.
7. Answer the financial literacy questions and scroll down to view results and click **"proceed"**.
8. Click on **get started** to start the application process.

9. Enter your phone number which should be registered in your name and national ID number to verify that you are the owner.
10. Read and understand the scholarship/loan terms and condition and **agree to proceed**.
11. Click request loan to view and verify your loan details.
12. Select your preferred loan payment option.
13. Click **"submit"** to complete the loan application. A pop-up message will appear to show that you have successfully applied. The loan serial number will also be displayed.
14. In due course, you will receive other notifications on awards and disbursements of upkeep and tuition loans and where applicable, bursary.
15. Contact HELB for any further assistance.

Please note:

This application is paperless. You are not required to print any form. A confirmation SMS with a loan application serial number is the evidence that you have applied. Kindly save the SMS for future reference. HELB does not charge any fee to access the loan application.

The closing date for the applications is 31st December 2024.

EMPOWERING DREAMS

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way USSD *642#
+254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE

Walemavu 300 Manderu wapata vifaa vya usaidizi

NA ADAN MOHAMED(KNA)

Zaidi ya Watu 300 Wenye Ulemavu katika Kaunti ya Manderu wana sababu ya kutabasa baada ya serikali ya kaunti hiyo kutoa vifaa aina mbalimbali ili kuwawezesha na kuwapa uhuru za kutembea.

Watu wenye ulemavu, ambao baadhi yao wamekuwa wamelazwa kwa miaka mingi, walipokea viti vya magurudumu, viti vya magurudumu vya chuma vinavyoweza kukunjwa vilivyoundwa kutumiwa na watoto, mikongojo, baiskeli za magurudumu matatu miongoni mwa vingine.

Mpango huu unalenga kutoa vifaa muhimu vya kuboresha ubora wa maisha, uhamaji, na uhuru wa watu wenye ulemavu.

Bi Sumeya Bishar, Waziri wa Kaunti wa Huduma za Kijamii na Jinsia alipokuwa akisambaza vifaa hivyo alisema hawatafungwa tena ndani ya nyumba zao kutokana na ukosefu wa vifaa vya kuwasaidia kutembea.

Aliongeza kuwa serikali ya kaunti itasambaza vifaa

mbalimbali vya usaidizi katika Kaunti ya Manderu na kuongeza kuwa masuala yanayohusu ulemavu yanayohusisha watu wenye ulemavu yatatatuliwa.

Bi Sumeya pia aliwahimiza watu wenye ulemavu na walezi wao kuchukua fursa ya vifaa vya usaidizi ili kuboresha maisha yao na kuwa na uhuru. Alisisitiza haja ya kusaidia vikundi hivi akisema vina talanta zisizo na kifani ambazo zikikuzwa zinaweza kuwaondoa katika umaskini.

“Serikali ya Kaunti ya Manderu imejitolea kuendeleza juhudi zake katika kutoa usaidizi na uwezeshaji kwa watu wenye ulemavu katika jamii yetu,” alisema akiongoza uzinduzi huo.

Ibrahim Ali aliwashukuru wafadhili kwa msaada huu akisema utaleta furaha kwa watu wengi zaidi wenye ulemavu.

Usaidizi huu utahakikisha kwamba watu wenye Ulemavu Manderu wataendelea na maisha yao ya kila siku kama watu wa kawaida. Tunashukuru,” alisema Ibrahim Ali.

Juhudi zaendelea kutafuta vyanzo vya maji chini ya ardhi katika kaunti kame

NA BERNADETTE KHADULI(KNA)

Serikali imetambua kaunti tano kame na kavu (ASAL) kutafuta chemchemi za maji chini ya ardhi ili kupata maji kwa wakazi wa maeneo hayo ambayo hayana usalama wa maji.

Bw Julius Korir, Katibu wa Idara ya Maji na Usafi wa Mazingira, alisema mpango huo unagali unaendelea Marsabit na kaunti zingine kumi na saba katika Mabonde ya Athi na Tana. Alisema kuwa zoezi hili litawezesha watafiti wa maji kubaini vyanzo vya maji chini ya ardhi na kiwango chake.

“Utafiti pia utabainisha wingi na ubora wa maji chini ya ardhi katika chemchemi hizi, na hii inaweza kuleta mabadiliko katika maeneo ya ASAL ambako maji ya juu ya ardhi ni haba,” Korir alisema. Alisema Kenya inakabiliwa na changamoto kubwa katika sekta ya maji, huku zaidi ya asilimia 40 ya watu wakikosa maji safi na vyoo vya kutosha.

Katibu alisema haya

katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Bw Kinyua Mware, wakati wa hafla ya kifungua kinywa ya vyombo vya habari kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa katika maeneo kavu ya Kenya iliyofanyika katika hoteli moja ya Nairobi.

Korir alipongeza mpango wa ‘Kufikia: Kuboresha Usalama wa Maji,’ unaofadhiliwa na Ofisi ya Maendeleo ya Jumuiya ya Madola (FCDO) kwa kipindi cha miaka 10, ambao umekuwa ukibadilisha maisha. Aliongeza kuwa kuongezeka kwa mahitaji ya maji na uhaba wa maji ni changamoto kubwa kwa maisha ya Wakenya.

Ushirikiano huu wa kimataifa umeleta pamoja vyuo vikuu vikiitoka Uingereza, Ethiopia, Bangladesh, na Kenya kwa dhamira ya kuhakikisha usalama wa maji kwa wale wanahitaji zaidi kulingana na matarajio ya nchi kufikia upatikanaji wa maji kwa wote ifikapo 2030, kama iliyoorodheshwa katika Katiba ya Kenya,



Katibu Julius Korir

Ruwaza ya Kenya 2030 na Lengo la 6 la Maendeleo Endelevu.

Alisema ongezeko la joto duniani, uchafuzi wa maji, ongezeko la watu, ukuaji wa miji, na usimamizi mbaya wa rasilimali za maji umezidisha shida ya maji. Katibu alisema kuwa uhaba wa maji unatarajiwa kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi, utoshelevu wa chakula, elimu, na afya, pamoja na kuzidisha mabadiliko ya hali ya hewa, ambayo alibainisha kuwa yamevutia hisia za umma. “Kwa hiyo ni muhimu kuhakikisha kuwa kuna usimamizi mzuri, bora na endelevu wa rasilimali za maji nchini ili kufikia usalama wa maji kwani mabadiliko ya hali

ya hewa yanazidisha hali kwa kubadilisha mzunguko wa kihaidrolojia hasa mwelekeo wa mvua,” alisema.

Alisema maeneo kame na nusu kame nchini yamo hatarini zaidi, huku ukame wa mara kwa mara na uhaba wa maji ukisababisha uhaba wa chakula, kuhama makazi na migogoro ya kijamii.

Alisema Serikali inania ya dhati ya kutatua changamoto zinazohusiana na uhaba wa maji na migogoro mingine inayohusiana na maji, ambayo alibainisha kuwa itafanyika kwa ukusanyaji na uhifadhi wa maji, ulinzi wa vyanzo vya maji, urejeshaji na ukarabati na ukusanyaji wa maji chini ya ardhi.



Ministry of Education
State Department For Technical, Vocational Education and Training

FINANCIAL YEAR 2024-2025

TVET STUDENTS' FIRST TIME SCHOLARSHIP, LOANS & BURSARY APPLICATIONS UNDER THE OLD AND NEW FUNDING MODELS

Higher Education Loans Board in conjunction with State Department For Technical, Vocational Education and Training invites applications for First Time 2024-2025 Financial Year TVET Scholarship, Loans and Bursary from Kenyan students admitted in National Polytechnics, Technical Training Institutes and Vocational Colleges under the Ministry of Education and are registered with Kenya Universities and Colleges Central Placement Service [KUCCPS] and members of the Kenya Association of Technical Training Institutions [KATTI].

Eligible students for the **NEW FUNDING MODEL**: Newly placed TVET Students applying for the First-Time TVET student scholarship and loan.

HOW TO APPLY:

1. Visit www.helb.co.ke to access the application portal to register, create and activate account. (Applicants are advised to use personal mobile numbers registered under their name and National Identification Number).
2. Log in, go to apply for Loan/Scholarship or both, select Artisan, Craft or Diploma then click on the 2024-2025 TVET First Time Loan and Scholarship Form.
3. Read and appraise yourself online on the Financial Literacy and appreciate the purpose of Higher Education Financing.

4. Access and fill the Scholarship and Loan application form online
5. Upon successful application and submission of the Scholarship and Loan application online, **YOU ARE NOT** required to print and submit any physical application to us. (**This is a paperless application process**)
6. You will be enabled to track the processing status of your application on the application portal.
7. For any assistance/support, kindly Contact HELB through contactcentre@helb.co.ke

Please ensure that you read, understand, and follow the instructions provided at the beginning of the online Scholarship and loan application process including reading and undertaking the HEF Financial Literacy Programme.

#KaaChonjo, HELB does not charge any fee to access the loan application. Report any form of extortion to authorities.

The closing date for the applications is **31st December 2024.**

EMPOWERING DREAMS

www.helb.co.ke Anniversary Towers University Way USSD *642#
+254711052000 contactcentre@helb.co.ke @HELBPAGE



Ministry of Education
State Department For Technical, Vocational Education and Training

FINANCIAL YEAR 2024-2025

TVET CONTINUING STUDENTS' SUBSEQUENT SCHOLARSHIP & LOAN APPLICATIONS UNDER THE OLD AND NEW FUNDING MODELS

The Higher Education Loans Board in conjunction with State Department for Technical, Vocational Education and Training invites applications for the **Second and Subsequent TVET Scholarship/Loan and Bursary for 2024-2025 Financial Year** from Kenyan continuing students admitted in National Polytechnics, Technical Training Institutes and Vocational Colleges under the Ministry of Education, registered with Kenya Universities & Colleges Central Placement Service [KUCCPS] and are members of the Kenya Association of Technical Training Institutions [KATTI].

Eligible students: Continuing Students enrolled in approved TVET courses and are applying for the **second and subsequent student loan.**

HOW TO APPLY:

1. Download the **HELB App** from **Google Play Store** or use USSD Code by dialing ***642#**
2. Register using your phone number to generate a PIN which you will use to log in.
3. Read, understand, and click to accept the **terms and conditions.**
4. Enter your (first name) as it appears on your national ID card, the ID number and valid email address to complete registration.
5. Click on the **scholarship or loans or loans & scholarship** tab and choose Certificate/Diploma. Then click **“apply”** on the Undergraduate second and subsequent scholarship and loan.

NB: Ensure the mobile number is registered under your name. **Please NOTE** that mobile numbers not registered in the student's name will not be able to proceed with the application.

6. Read and understand the process tutorial and proceed to read the financial literacy guide.
7. Answer the financial literacy questions and scroll down to view results and click **“proceed”**.
8. Click on **get started** to start the application process.
